## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI SEPTEMBA, 2021 NA MWELEKEO KWA MWEZI OKTOBA, 2021.

**Dondoo za tathmini ya Septemba, 2021 na mwelekeo wa Oktoba, 2021:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Septemba, 2021 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Oktoba, 2021 nchini.

- Katika kipindi cha mwezi Septemba, hali ya baridi ya kawaida iliripotiwa katika baadhi ya maeneo nchini. Kiwango cha chini zaidi cha joto kiliripotiwa katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, kanda ya kusini na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali unaofikia km 40 kwa saa viliripotiwa katika maeneo ya pwani.
- Katika mwezi Oktoba, 2021 mvua za Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, maeneo machache ya Ukanda wa ziwa Victoria na pwani yanatarajiwa kuendelea kupata vipindi vya mvua. Viwango vya joto vinatarajiwa kuongezeka katika baadhi ya maeneo nchini.

## 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2021.

Katika kipindi cha mwezi Septemba, hali ya baridi iliripotiwa katika baadhi ya maeneo nchini hususan nyanda za juu kusini magharibi, kanda ya kusini pamoja na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Katika kipindi cha mwezi Septemba, vituo vya hali ya hewa Uyole (kilichopo mkoa wa Mbeya) na Igeri (kilichopo mkoa wa Njombe) viliripoti viwango vidogo vya joto la chini kati ya nyuzi joto 7 na 13. Kwa upande vipindi vya upepo mkali unaofikia km 40 kwa saa viliripotiwa katika baadhi ya

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**
*727B –00/2019*

maeneo nchini. Aidha, baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria na pwani yalipata vipindi vya mvua.

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI OKTOBA, 2021

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa chini ya wastani. Aidha, Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika maeneo ya upande wa magharibi mwa Bahari ya Hindi wakati upande wa mashariki mwa Bahari ya Hindi unatarajiwa kuwa na joto la bahari la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kupunguza upepo wenye unyevunyevu unaovuma kuelekea maeneo ya pwani. Hali ya joto la wastani hadi chini kidogo ya wastani inatarajiwa eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki karibu na pwani ya Angola. Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo kuvuma kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi. Kwa upande mwingine, hali ya joto la wastani hadi chini kidogo ya wastani katika maeneo ya kusini mwa Afrika inatarajiwa kuendelea kupunguza vipindi vya baridi.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2021

Kwa ujumla mvua za Vuli, 2021 zinatarajiwa kuanza kwa kuchelewa na kusuasua katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki. Kwa maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Hali ya baridi la kawaida inatarajiwa kuendelea hususan katika maeneo ya miinuko ya

nyanda za juu kusini magharibi na kaskazini mashariki. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa pwani. Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 hadi 25 katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko ya mkoa wa Tanga pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Morogoro yanatarajiwa kuwa na viwango chini ya nyuzi joto 18.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa hususan katika maeneo machache ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 hadi 18 katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 12.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 hadi 20 katika maeneo mengi. Hata hivyo maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango vya chini ya nyuzi joto 16.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 hadi 22 katika maeneo mengi.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea. Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 hadi 20 katika maeneo mengi.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 hadi 16 katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko pamoja na mikoa ya Njombe na Mbeya yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 10.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Hali ya ukavu inatarajiwa pamoja na vipindi vichache vya mvua katika maeneo machache ya mwambao wa pwani. Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 hadi 24 katika maeneo mengi.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 hadi 20 katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 16.

**2.3 MATARAJIO KWA MWEZI NOVEMBA, 2021.**

Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2021 vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, hali ya joto inatarajiwa kuwa ya kawaida katika maeneo mengi ya nchi.

**2.4 USHAURI**

Vipindi vichache vya mvua vinavyotarajiwa vinaweza kusababisha upungufu wa unyevunyevu katika ardhi hususan katika maeneo yanayopata mvua za Vuli. Wakulima pamoja na jamii kwa ujumla wanashauriwa kupata na kufuata ushauri wa maafisa ugani juu ya matumizi sahihi ya mvua hizo.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Oktoba, 2021 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**